

Serikali kujikita utafiti wa maziwa

Na Zuwena Shame

Serikali imesema imedhamiria kushirikiana na sekta binafsi ili kufanya utafiti mbalimbali utakazosaidia sekta ya maziwa nchini kuwa na tija na kuongeza pato la mfugaji na taifa kwa ujumla.

Aidha utafiti huo utawezesha zao la maziwa kwa kusaidia a kuongeza mnyororo wa thamani kwa kutengeneza bidhaa za zitokanazo na maziwa.

Hayo yalisema jijini Dar es Salaam juzi na Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (anayeshughulikia sekta ya mifugo), Prof. Elisante Ole Gabriel, wakati wa ghafla ya kukabidhi vyeti kwa washindi wa shindano la wauza pembejeo za kilimo lillioendeshwa na tassisi ya AgResults katika mikoa ya Pwani, Tanga, Dar es Salaam na Morogoro.

Ole Gabriel alisema kwa sasa Tanzania inashika nafasi ya pili kwa uzalishaji wa maziwa Afrika, hivyo ni muda sahihi kuweka nguvu katika sekta hiyo kwa kufanya utafiti utakaosaidia mchakato mzima wa mnyororo wa thamani.

Alisema kuwa katika nchi mbalimbali sekta ya maziwa imekuwa inchangia pato la taifa, hivyo hata Tanzania inaweza kuiga mafanikio hayo, kwa kukaribisha wawekezaji na kuzalisha bidhaa nydingi za maziwa.

Aliongzea kuwa takwimu zinaonyesha sekta ya maziwa inaongezeka kila mwaka na kuchangia pato la taifa kwa asilimia 7.4.

Mratibu wa mradi wa AgResults, Neema Mrema, alisema wafugaji wengi wa ng'ombe wa maziwa nchini wanakabiliwa na vikwazo hivyo kusababisha vya uzalishaji duni wa maziwa, hilo linasababishwa na kutopatikana pembejeo bora na huduma za ushauri na ugani.

Nipashe uk.10

Julai 2.2021